

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

680


UALIMU ELIMU YA AWALI

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Umepewa jukumu la kutafuta walezi wa watoto wa kituo cha Elimu ya Awali kijijini kwako. Utazingatia sifa zipi katika kutekeleza jukumu hilo? Toa hoja nne.
2. Mwalimu Mkuu amewataka walimu wote wa Elimu ya Awali kubainisha sifa za mbinu watakazotumia katika ufundishaji na ujifunzaji. Eleza kwa ufupi sifa nne watakazozingatia katika kufanya kazi hiyo.
3. Mambo gani yanayofanyiwa tathmini katika mfumo wa Elimu ya Awali? Bainisha mambo manne.
4. Umeteuliwa kutoa semina kwa walimu wa Elimu ya Awali juu ya hatua muhimu za kufuata wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa michezo. Ainisha kwa ufupi hatua kuu nne utakazowashirikisha walimu hao.
5. Eleza kwa ufupi mambo manne yanayohusu ufundishaji yanayojumuishwa kwenye mtaala wa Elimu ya Awali.
6. Ni mambo gani ya kuzingatia kabla ya kutoa ushauri nasaha wa vikundi kwa watoto wa Darasa la Awali? Bainisha mambo manne.
7. Eleza kwa ufupi nyanja nne za makuzi ya mtoto.
8. Ni kwa namna gani mbinu ya ziara hukuza matumizi ya milango ya fahamu kwa watoto wa Elimu ya Awali? Toa hoja nne.
9. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa ufupi mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali.
10. Chambua kwa ufupi hatua nne za ukuaji wa mtoto kiakili kama zilivyotolewa na Jean Piaget.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Ukiwa kama mwalimu wa watoto wa Elimu ya Awali, eleza ni kwa namna gani utawashirikisha wadau wa elimu kutambua mahitaji ya watoto hao. Toa hoja tano.
12. Kwa kutumia hoja tano, oneshwa namna utakavyomtambua mtoto mwenye ulemavu wa akili.
13. Ni muhimu kwa mwalimu kufanya tathmini ya maendeleo ya somo katika Elimu ya Awali. Eleza kwa kina hatua tano utakazozingatia ili kuweza kufanikisha tathmini hiyo.
14. Chambua maeneo sita ya ujifunzaji yaliyobainishwa katika mtaala wa Elimu ya Awali ambayo mwanafunzi anapaswa kujifunza.